



**OFISI YA MKUU WA MKOA WA MARA  
(IDARA YA MAENDELEO YA USHIRIKA)**



**MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA**

**Muda wa kutoa Huduma muhimu kwa Mteja kwenye Sekta ya Ushirika**

Tutashughulikia huduma muhimu haraka iwezekanavyo na wakati wote katika viwango vya muda vifuatavyo:-

- ❖ Kusajili au kufuta Vyama vya Ushirika vya Msingi: **siku 90**
- ❖ Kusajili mikopo, rehani mbalimbali na barua ya rehani ya bidhaa au mazao: **Siku 3**
- ❖ Kuratibu ufilisi wa Vyama vya Ushirika vya Msingi: **Miezi 12**
- ❖ Kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni ya Vyama vya Ushirika vya Msingi: **Miezi 12**
- ❖ Kuandaa na kusambaza Sheria na maagizo ya Mrajis: **siku 14**
- ❖ Kusuluhisha migogoro ndani ya Chama cha Ushirika cha Msingi: **Siku 60**
- ❖ Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sheria ya Ushirika: **miezi 12**
- ❖ Kufanya mapitio ya makadirio ya mapato na matumizi ya Vyama vya Ushirika vya msingi: **Siku 60**
- ❖ Kuandaa kanuni za Fedha na Mwongozo wa Uhasibu kwa Vyama vya Ushirika vya Msingi: **Siku 90**
- ❖ Kusaidia tafsiri ya Hesabu zilizokaguliwa katika mikutano ya mwaka ya Vyama vya Ushirika vya Msingi: **Siku 5**
- ❖ Kuandaa mchanganuo wa fedha/ Hali ya kiuchumi ya Vyama vya Ushirika, Vyama kilele na shirikisho la Vyama Ushirika: **Siku 30**
- ❖ Kufuatilia na kufanya tathmini juu ya matumizi bora ya mwongozo wa ukaguzi: **Miezi 12**
- ❖ Kufanya ukaguzi maalumu wa Vyama vya Ushirika vya Msingi: **Siku 21**
- ❖ Kufanya ukaguzi kawaida wa Vyama vya Ushirika, Vyama kilele na Shirikisho la Vyama: **Siku 21**
- ❖ Kuratibu na kufuatilia shughuli za COASCO na Wakaguzi wengine wa nje: **Miezi 12**

- ❖ Kusimamia ufungaji wa Hesabu za Vyama vya Ushirika vya Msingi: *Siku 14*
- ❖ Kuongeza uwezo na kufundisha Wakaguzi wa Ushirika, wafanyakazi na Taasisi za Fedha za Ushirika: *Miezi 12*
- ❖ Kuhamasisha wanachama kuweka akiba na kuunda taasisi za fedha: *Miezi 12*
- ❖ Kufuatilia na kutathmini utendaji wa Taasisi za Fedha za Ushirika: *Miezi 12*
- ❖ Kusaidia upatikanaji wa Mitaji na kuviunganisha Vyama vya Ushirika vya Msingi na Taasisi za Fedha: *Siku 60*
- ❖ Kuratibu mafunzo ya Ushirika yatolewayo katika Taasisi mbalimbali: *Miezi 12*
- ❖ Kuwezesha maendeleo na utekelezaji wa Elimu ya Ushirika kwa Wanachama, Viongozi na Watumishi: *Miezi 12*
- ❖ Kuunganisha makundi mbalimbali yanayokuza Ushirika: *Miezi 12*
- ❖ Kuandaa Programu ya mafunzo kwa Vyama vya Ushirika: *Siku 90*
- ❖ Kuandaa majibu ya maswali ya Bunge: *Siku 14*
- ❖ Kuandaa na kufanya mapitio ya mwongozo wa uwekezaji na utendaji wa Vyama vya Ushirika vya Msingi: *Siku 21*